

9. Things Fall Apart

9. Things Fall Apart

Vitabu100Siku100 na Kocha Dr Makirita Amani.

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha TISA kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.

Things Fall Apart ni riwaya iliyoandikwa na Chinua Achebe inayohusu maisha ya tamaduni za Afrika kabla na baada ya kuja kwa wamishioniari.



Okonkwo ni shujaa ambaye umaarufu wake ni mkubwa kwenye kijiji chake cha Umuofia na hata vijiji jirani.

Alipata umaarufu wake baada ya kumshinda kwenye mieleka mpiganaji aliyekuwa maarufu ambaye hakuwahi kushindwa kwa miaka saba.

Baada ya hapo Okonkwo aliendelea kufanya makubwa na kupata mafanikio makubwa.

Ana shamba kubwa la viazi, ana wake watatu na ana vyeo viwili vya kimila, hatua ambayo ni kubwa kwa umri wake.

Katika jamii yao, mtu haheshimiwi kwa umri, bali kwa mafanikio aliyopata na wanayo kauli inayosena mtoto akinawa mikono yake, atakula na wafalme, Okonkwo ni mmoja wa walionawa mikono mapena na kula na wafalme.

Baba yake Okonkwo hakuwa na mafanikio yoyote, maisha yake yalikuwa ni ya aibu. Hakupenda kazi bali starehe, alikuwa na madeni kwa majirani wote.

Alipenda kupiga filimbi na msimu wa mavuno ndiyo aliupenda zaidi.

Alikuwa akipata pesa anaitumia yote kwa kula na kunywa. Alikuwa na msemo wake kwamba kila akiona mdomo wa mtu aliyekufa, aliona ni ujinga mtu kutokutumia alichonacho wakati yuko hai.

Okonkwo hakijivunia kuwa na baba wa aina hiyo, hivyo alipambana kujenga maisha ya mafanikio na heshima kwake.



Usiku mmoja la mgambo linalia na tangazo linatolewa kwa wanaumw wote kukutana siku inayofuata. Okonkwo anatumia usiku kucha kutafakari mkutano huo wa dharura ni wa nini, je ni vita au nini.

Hakuwa anahofia vita, yeye ni mmoja wa mashujaa wa kivita ambaye kwa umri wake ameshaleta vichwa vitano alivyowakata watu kwenye vita.

Asubuhi inafika na wanahudhuria mkutano, wanapewa taarifa kwamba mwanamke wa kijiji cha Umuofia ameuawa kwenye kijiji cha Mbaino alipoenda sokoni.

Taarifa hiyo inawapa watu hasira. Wanafikia maamuzi ya kutuma ujumbe kwenye kijiji hicho, wachague vita au kulipa kijana mdogo na mwanamke bikira.

Okonkwo anapeleka ujumbe, kijiji wanakubali kulipa fidia maana Umuofia inaogopeka kwa vita.

Wanarudi na kijana na mwanamke bikira, mwanamke anakabidhiwa kwa mume ambaye mke wake ameuawa na kijana ni mali ya kijiji, ila kwa sasa inaamuliwa aishi kwa Okonkwo.

Kijana anaitwa Ikemefuna na anakaa nyumbani kwa Okonkwo ambaye anamchukulia kama mtoto wake.

Okonkwo amekuwa akiendesha familia yake kwa ukali, amekuwa akiogopwa sana na wake zake na watoto pia.

Japo kwa nje Okonkwo aliweza kuonekana kama katili, ndani yake hakuwa hivyo. Maisha yake yalitawaliwa na hofu kubwa ya kushindwa na kuonekana ni dhaifu. Hakuwa anaogopa vita, wala mapambano yoyote. Ila kila alipokumbuka maisha ya baba yake, hakutaka kabisa kuwa kama yeye. Hivyo aliazimia kuchukia vitu vyote ambavyo baba yake alipenda. Na vitu viwili vikubwa alivyoondoa

kabisa kwenye maisha yake ni upole na uvivu.

Okonkwo alifanya kazi kuanzia kunapambazuka mpaka jua linazama, hakuwa anachoka wala kupumzika.

Lakini familia yake haikuonekana kuweza kufanya kazi kama yeye.

Mtoto wake wa kwanza aitwaye Nwoye hakuonekana kuweza kazi kama Okonkwo alivyotaka, hivyo alimchukulia ni mvivu na kila wakati alimsema na kumwadhibu.

Nwoye alionekana kuwa na uso wa huzuni wakati wote.

Kifamilia Okonkwo alikuwa na mafanikio makubwa, alikuwa na shamba kubwa, eneo aliloishi alijenga uzio na ndani yake kulikuwa na nyumba yake, nyumba tatu moja kwa kila mke wake na nyumba yake ya kufanya ibada na kutoa sadaka kwa mizimu.

Okonkwo alikuwa na watoto 8 kwa wake zake watatu. Alipopewa jukumu la kukaa na Ikemefuna alimkabidhi kwa mke wake wa kwanza.

👉3

Okonkwo hakuanza maisha kwa urithi wowote kutoka kwa baba yake. Baba yake alikuwa mvivu, hakuwa na shamba wala hakulima.

Alianzia chini kabisa, bila ya kuwa na chochote.

Alianza kwa kushirikiana kilimo na wengine, lakini aliona njia hiyo itamchelewesha.

Hivyo aliamua kuandaa shamba na kwenda kwa mzee tajiri wa kijiji hicho kwenda kumwomba mbegu.

Aliandaa mvinyo na kwenda nao na baada ya kunywa kwa pamoja alieza nia yake.

Mzee yule alimjibu vijana wengi wamekuwa wanakuja kwake wakitaka mbegu, lakini amekuwa akiwakatalia kwa sababu anajua ni wavivu. Ila atamkubalia Okonkwo kwa sababu hata kwa mwonekano tu, ana uhakika ni mchapakazi.

Okonkwo anapewa mbegu nyingi kuliko alivyotegemea, lakini kwa bahati mbaya mwaka huo unakuwa mbaya kuliko miaka yote kwenye kilimo.

Anapata hasara kubwa, lakini hakati tamaa. Na amekuwa anajiambia kama aliweza kuvuka mwaka huo mbaya, hatakuja kushindwa au kukata tamaa.

Licha ya kuanzia chini kujenga maisha yake, Okonkwo pia alikuwa na utegemezi mkubwa, mama yake na dada zake walimtegemea yeye, hilo lilimpa mzigo mkubwa pia.

Lakini hakuruhusu liwe kikwazo kwake, alipambana ili kujenga maisha tofauti na ya baba yake.

👉4

Okonkwo hakuwa na huruma wala uvumilivu kwa watu ambao hawakuwa wamefanikiwa, aliwaona ni wazembe.

Hilo lilifanya baadhi ya watu waone ana kiburi cha mafanikio na kumtaka awe mnyenyekevu kwa kuwa ana bahati.

Lakini mafanikio ya Okonkwo hayakutokana na bahati, bali juhudi kubwa alizoweka.

Ikemefuna ameendelea kukaa kwenye familia ya Okonkwo kwa miaka mitatu, wanajebga ukaribu na Nwoye, mtoto wa kwanza wa Okonkwo. Muda mwingi wanakuwa pamoja.

Okonkwo anaonekana kumpenda na kumkubali sana Ikemefuna kama mtoto wake, japo haoneshi hilo waziwazi. Kwa Okonkwo kuonesha hisia wazi ni udhaifu mkubwa.

Okonkwo anawafundisha kazi watoto hao wawili na kuwaambia hapendi wavivu, anasema kama mtoto wake akishindwa kujenga maisha yake mwenyewe, atamuua kwa mikono yake.

Okonkwo anafanya kosa la kumpiga mke wake kwenye wiki ya amani, hiyo ni wiki moja kabla msimu mpya wa kilimo haujaanza. Okonkwo anaadhibiwa kwa kosa hilo, ila wengi wanamsema vibaya, wanasema sifa zimempanda kichwani.

👉5

Ni msimu wa mavuno, kipindi ambacho hakuna kazi bali sherehe na mapumziko.

Okonkwo huwa hapendi kipindi hiki, huwa hapendi kukaa bila kazi yoyote.

Okonkwo pia ni mtu ambaye huwa hawezi kujizuia hasira zake na akishakuwa na hasira lazima atafute mtu wa kumpiga hata kama hahusiani na hasira hizo.

Siku moja mke wake wa pili alimjibu vibaya na alijikuta akimlenga na bunduki, risasi ikamkosa. Siku ya kwanza ya sherehe za mavuno ni ya kuwaalika ndugu na jamaa, familia ya Okonkwo inapika chakula kingi na ndugu wa wake zake wanajumuika nayo kwenye siku hiyo. Siku ya pili ya sherehe huwa kunakuwa na pambano la mieleka, ambapo watu wengi hupenda kuhudhuria. Mke wa pili wa Okonkwo anapenda sana mieleka na siku hii anaandaa chakula mapema ili yeye na binti yake pekee aitwaye Ezinma waweze kwenda kwenye mieleka.

👉6

Ni siku ya mieleka, watu wamekusanyika kwenye uwanja ambapo michezo hiyo inafanyika. Mke wa pili wa Okonkwo anakutana na mwanamke aliyemsaidia akapata mtoto pekee aliyenaye. Anamuuliza mtoto anaendeleaje, anamjibu vizuri, anamuuliza ana miaka mingapi anamjibu 10. Anamwambia huenda akaishi na asife, maana wengi wakishavuka miaka 6 huwa wanaishi. Mwanamke huyo anamuuliza kama ni kweli Okonkwo alitaka kumuua kwa risasi, anajibu ndiyo. Michezo ya mieleka inaanza, wanatangulizwa watoto, kisha timu za mieleka na mwisho wapiganaji wakuu wanaingia uwanjani. Mpambano nakuwa mkali kati ya Ikezue na Okafo na Okafo anashinda. Anabebwa na kuzungushwa huku watu wakiimba ni shujaa.

👉7

Ikemefuna amekaa na familia ya Okonkwo kwa miaka mitatu sasa, amekuwa kama sehemu ya familia na amekuwa anamuita Okonkwo baba. Wamekuwa na ukaribu na mtoto wa kwanza wa Okonkwo ambaye ni Nwoye na amembadilisha kwa kiasi kikubwa, kitu ambacho Okonkwo anakifurahia. Nwoye siyo mvivu na mzembe tena kama alivyokuwa zamani na vijana hao wawili hutumia muda mwingi na Okonkwo kumsaidia kazi zake. Okonkwo anajivunia kuwa na kijana anayekua kama mwanaume, atakayeweza kuendesha familia yake vizuri. Siku moja mzee wa kijiji anakuja kwa Okonkwo na kutaka kuongea naye faragha. Anamwambia uongozi wa kijiji umeamua Ikemefuna atolewe kafara. Ila kwa kuwa amekuwa anamuita Okonkwo baba, basi asishiriki kwenye kafara hiyo. Taarifa hizo zinamhuzunisha Okonkwo anamwambia Ikemefuna kwamba siku inayofuata anarudishwa kijijini kwao. Familia nzima inasikitika kwa hilo. Siku inayofuata watu wanakuja nyumbani kwa Okonkwo na wanaondoka na Ikemefuna, Okonkwo anaongozana nao. Wanatembea mpaka katikati ya msitu ambapo mtu mmoja anatoa panga kumkata Ikemefuna, lakini anamkosa, Ikemefuna anakimbilia kwa Okonkwo na kumuita baba nisaide, wanataka kuniua. Okonkwo anatoa panga lake na kumuua, anafanya hivyo ili asionekane dhaifu. Anarudi nyumbani akiwa na huzuni kubwa, Nwoye anapomuona baba yake hisia zinamjia ndani yake kwamba Ikemefuna ameuliwa. Aliwahi kupata hisia kama hizo aliposikia sauti ya watoto wachanga wanalia msituni na kuambiwa mapacha wakizaliwa huwa wanapelekwa msituni na kuachwa huko wafe, maana ni kisirani kwa kijiji.

👉8

Okonkwo hajala chochote kwa siku mbili, anakunywa pombe na kukaa ndani muda wote. Anamuita Nwoye akae naye lakini anamhofia, akishamuona baba yake anasinzia anatoroka. Siku ya tatu anaagiza mke wake wa pili amtengenezee chakula, mtoto wake Ezinma anamletea chakula na kumwambia baba hujala kwa siku mbili, inabidi umalize chakula chote. Okonkwo anajiambia ndani yake natamani sana huyu angekuwa mtoto wa kiume, angefaa zaidi kuwa mrithi wangu. Baada ya kula Okonkwo anatafuta kitu cha kufanya ili kuondoa mawazo ya Ikemefuna. Wako kwenye msimu wa mapumziko hivyo hakuna kazi za shamba.

Mawazo ya Ikemefuna hayamtoki kwenye akili yake. Anajiambia kwa nini anakuwa dhaifu kama mwanamke, ameuwa watu watano kwa mkono wake kwenye vita, kwa nini kumuua kijana huyo imsumbue?

Anatoka kwenda kumtembelea mzee mwingine aitwaye Obierika, anafika na kupokelewa. Obierika anamwambia alikuwa anapanga kuja kwake kumweleza ugeni alionao wa watu wanaokuja kutoa mahari kwa binti yake

Wanakaa na kuongea, Okonkwo anamuuliza kwa nini hakushiriki kwenye kumtoa kafara Ikemefuna, Obierika anamwambia alikuwa na mambo mengine muhimu ya kufanya. Okonkwo anamwuliza haoni watu watachukulia hilo kama udhaifu? Obierika anamwambia kila mtu kwenye kijiji hicho anajua ujasiri wake kwenye vita, hahitaji kuthibitisha hilo kwa kushiriki mauaji ya kijana mdogo.

Obierika anamwambia Okonkwo kama ingekuwa ni yeye, asingeshiriki kwenye zoezi hilo, maana litaleta laana kwa kijiji kizima. Okonkwo anamwambia mizimu ndiyo ilichagua hivyo, Obierika anamwambia ni kweli, ila hakukuwa na ulazima wa yeye kushiriki.

Wanaendelea na mazungumzo mengine, anamuona mtoto wa Obierika aitwaye Maduka, ambaye ni mwanamieleka na jasiri na kusema angetamani mtoto wake naye awe hivyo.

Wageni wanakuja, wanakula, kunywa na kikubaliana mahari kisha wanaendelea na mazungumzo mengine.

👉9

Bado Okonkwo anapata shida ya kulala usiku, mara nyingi anashtuka usingizini na kuwa na mawazo kuhusu tukio la kumtoa kafara Ikemefuna.

Asubuhi na mapema mke wake wa pili anakuna kumuamsha na kumwambia Ezinma anaumwa sana. Okonkwo anaenda haraka na kukuta mtoto huyo ana homa kali, anachukua panga na kwenda kukata miti ya dawa, anarudi yano, wanaichemsha na kumfukiza.

Baada ya kufukizwa Ezinma analala usingizi.

Ezinma ni mtoto pekee wa mke wa pili wa Okonkwo aliye hai. Mwanamke huyo alizaa watoto 10 na tisa walifariki wakiwa wadogo.

Amefanyiwa kila aina ya dawa, lakini haijasaidia.

Wanaamini mtoto wake wa kwanza ndiye anayewaua watoto wengine, baada ya kufa amekuwa anarudi kwenye tumbo la mama yake na kizaliwa tena kisha kufa.

Ezinma ndiye mtoto pekee aliyevuka miaka mitatu, mara kadhaa amewahi kuumwa, ila akafanyiwa dawa na wakaamini wamevunja uhusiano wake na mtoto wa kwanza.

Alipovuka miaka 6 wengi waliamini hatakufa kama wenzake, bali ataishi.

👉10

Ni siku ya kesi, watu wamekusanyika kwenye uwanja wa mkutano. Wanaume wako mbele na wanawake wako nyuma, kama wanachungulia na tukio haliwahusu.

Kesi huwa zinaendesha na mizimu tisa ya familia zilozoasisi Umuofia, hivyo mizimu tisa inaingia kwenye uwanja.

Wake wa Okonkwo wanashangazwa kuona moja ya mizimu hiyo unatembea kana Okonkwo, lakini pia yeye haonekani walipokaa wazee wengine wa cheo kama chake.

Lakini hawasemi lolote kuhush hilo.

Wanaamua kesi ya mtu ambaye mke wake amechukuliwa na ndugu zake kwa sababu alikuwa anampiga sana. Akaenda kuwaambia wanrudishie mahari wakakataa.

Mizimu inajadiliana na kuamua watu hao wapataane na mke arudi kwa mume.

Baadhi ya wazee wanaulizana mbona maamuzi hayo hayajaweka uzito kwa hatari ambayo mwanamke huyo anayo kwa kurudi kwa mume wake. Wanakubaliana kwamba maamuzi yamefanyika kumridhisha mwanaume, maana asingekubali kingine tofauti na hicho.

👉11

Ni usiku tulivu na wenye giza, Okonkwo yuko kwenye nyumba yake na wake zake wako kwenye nyumba zao wakiwasimulia watoto wao hadithi mbalimbali.

Mke wa pili na binti yake Ezinma wanasimuliana hadithi ya kobe na ndege. Ghafla wanasikia sauti ya mtabiri wa kijiji ikija kwa Okonkwo na kusema miungu inataka kumuona Ezinma usiku huo. Okonkwo anamwambia muda huo mtoto amelala, mtabiri huyo anamwambia asijaribu kubishana na miungu. Anaenda kwenye nyumba ya mke wa pili, anaagiza mtoto atolewe na kumbeba. Mtoto analia sana, lakini mama yake anamwambia asiwe na wasiwasi, atakuwa salama. Mama wa mtoto anamwambia mtabiri ataongozana na mwanaye, mtabiri anamwambia hilo haliruhusiwi. Baada ya mtabiri yule kuondoka mama wa mtoto anashindwa kuvumilia na kumfuata kwa nyuma, wanatembea usiku kucha mpaka wanafika kwenye pango, mtabiri na mtoto wanaingia kwenye pango hilo, mama anajiambia atasubiria hapo nje, ila akisikia kelele za mtoto wake kudhurika, ataingia kuzuia hilo. Anageuka na kumuona Okonkwo ambaye pia alifuata nyuma, wanasubiri pamoja nje ya pango hilo.

👉12

Wakiwa pale nje ya pango ni asubuhi kumeshakucha, mtabiri yule anatoka amembeba Ezinma na kurudi kijijini. Anaenda mpaka kwenye nyumba ya mama wa mtoto, anamlaza na kuondoka. Okonkwo na mke wake wa pili wanarudi, wamechoka na wanataka kupumzika. Siku hiyo ni shereye ya kuolewa mtoto wa Obierika ambaye walienda kupokea mahari siku zilizopita. Mke wa pili wa Okonkwo anawaombe wenzake wamuombee udhuru kwamba atachelewa maana amechoka sana. Sherehe inakuwa kubwa na ya kufana, watu wanakula na kunywa na kusaza. Waoaji wanaondoka na mke wao.

👉13

La mgambo linalia, taarifa ya msiba inatangazwa, mmoja wa wazee wa kijiji aitwaye Ezeudu amefariki dunia. Taarifa hiyo inamshtua sana Okonkwo, Ezeudu ndiye aliyemtahadharisha asishiriki kafara ya Ikemefuna. Ezeudu alikuwa na cheo cha juu lakini pia ndiye alikuwa mzee kuliko wote. Hivyo mazishi yake yalikuwa ya kishujaa, watu kutoka sehemu mbalimbali walishiriki. Bunduki zilipigwa hewani kama ishara ya heshima. Katika shughuli hizo za mazishi, kwa bahati mbaya bunduki ya Okonkwo inafyatuka na kumuua mtoto wa Ezeudu. Jambo hilo ni baya kwa tamaduni zao, anayefanya hivyo anapaswa kuuawa au kukimbia kijiji na asirudi kwa miaka 7. Okonkwo hana budi, inambidi aondoke kwenye kijiji hicho na kwenda kijiji alikotoka mama yake, kijiji kinachoitwa Mbanta. Rafiki yake Obierika anawaza sana kuhusu tamaduni hizo na kushindwa kupata jibu, anakumbuka wakati alilazimika kupeleka watoto wake mapacha porini kwa sababu jamii inaona ni kisirani. Na sasa anamkosa rafiki yake kwa kitu alichofanya bila kukusudia. Haridhishwi na hayo, ila pia anaona ni mema kwa mustakabali wa jamii nzima, japo kwa mmoja mmoja siyo mema.

👉14

Okonkwo na wake zake watatu pamoja na familia wanafika kijiji cha Mbanta alikozaliwa na kuzikwa mama yake. Mjomba wake anayeitwa Uchendu anampokea na kwa huzuni aliyokuwa nayo Okonkwo anajua mambo si mazuri. Okonkwo anamwelezea kilichotokea, anamuelewa na kumpokea. Anampa shamba na mahali pa kujenga nyumba zake, anajenga nyumba yake na za wake zake watatu pamoja na eneo la miungu wake.

Okonkwo ni kama anaanza maisha upya, ila safari hii hana hamasa kama aliyokuwa nayo awali. Anaonekana amekata tamaa na kila wakati ana huzuni kubwa. Lengo lake ilikuwa aje kuwa mmoja wa wazee wa kijiji mwenye cheo cha juu kabisa, ndiyo maana alijituma sana. Lakini sasa yuko uhamishoni kwa miaka 7, anaona hilo haliwezekani tena. Uchendu anagundua hilo kuhusu Okonkwo anajaribu kuongea naye lakini haisaidii. Uchendu anaamua kuitisha mkutano na watoto wake wote pamoja na Okonkwo, anawaeleza Okonkwo yuko pale kwa miaka saba. Anawaeleza kwa nini mtu anaenda uhamishoni upande wa mama na kwa nini wanawake huwa wakifa wanarudishwa kuzikwa kwao. Mara zote mambo yanapokuwa mazuri watoto hukaa upande wa baba, lakini mambo yakiwa mabaya watoto hukimbilia kwa mama. Hivyo wamama huzikwa kwao ili watoto wapate pa kukimbilia. Uchendu anamwambia Okonkwo kwamba kama ataendelea na hali yake ya huzuni, atamkasirisha mama yake aliyekufa na maisha yake hapo hayatakuwa mazuri. Anamwambia yaliyomkuta siyo mabaya kuliko ya wengine, anampa mfano kwamba yeye alikuwa na wake 6 na wote wamekufaza, amezika watoto 22. Anampa mifano ya wengine ambao wanaishi uhamishoni milele. Hivyo anamtaka aache kuhuzika na kukata tamaa, miaka 7 itaisha na atarudi kwenye kijiji chake.

👉15

Mwaka wa pili Okonkwo akiwa uhamishoni rafiki yake Obierika anamtembelea. Amebeba mifuko yenye fedha ambayo anamwambia ameuzia mazao aliyoyaacha, huku mengine akiwapa watu wapande na kurejesha kwa faida. Anamwahidi atakuwa anafanya hivyo mpaka atakapomaliza adhabu yake na kurudi. Anampa habari kwamba kwenye kijiji kimoja watu wameuawa. Alikuwa mzungu mmoja akiwa na gari, wakauliza mizimu ikawaambia huyo ni mtu hatari na hivyo wakamuua. Siku nyingi baadaye wakaja wazungu wengine wameambatana na vijana wa vijiji jirani na kuwashambulia watu kwa risasi wakiwa sokoni. Okonkwo na Uchendu wanasikitika kwa hilo, na kusema walifanya jambo la kipumbavu kumuua mzungu huyo.

👉16

Miaka miwili baadaye Obierika anamtembelea tena Okonkwo. Anamueleza mambo siyo mazuri huko Umuofia, kwani wamishionari wamekuwa wengi, wamejenga makanisa na kuna watu wamejiunga na dini yao. Japo wazee wa kimila wanaona wamishionari hao hawana madhara, kwani waliojiunga nao ni watu wasio na vyeo wala heshima kwenye kijiji. Kilichomshtua Obierika ni kumuona Nwoye, mtoto wa Okonkwo akiwa na wamishionari hao, alipomuuliza amamjibu amejunga nao. Alipomuuliza kuhusu baba yake Okonkwo akamjibu siyo baba yake. Okonkwo hakutaka kuongea chochote kuhusu Nwoye, ila mke wake alimueleza Obierika kilichotokea. Wamishionari walikuja pia kwenye kijiji hicho cha Mbanta na kueleza wameleta taarifa za Mungu wa kweli na hivyo watu waachane na miungu ya uongo wanayoamini. Walieleza jinsi mungu huyo ni wa upendo, ambaye haruhusu watu kuuana. Wanakijiji wengi waliwapuuza na kuwaona kama wamishionari hao wamechanganyikiwa, wanawaitaje miungu wao wa uongo? Lakini Nwoye alikubali kujiunga na wamishionari hao, kwa kuwa aliona ndiyo sehemu pekee inayogusa yale ambayo alikuwa hakubaliani nayo kwenye jamii yake, mfano kuuawa kwa Ikemefuna.

👉17

Wamishionari waliomba eneo la kujenga kanisa lao. Wazee wa kimila wakaona hiyo ni fursa ya kuwaondoa, hivyo wakawapa eneo kwenye msitu wa mizimu, ambapo maiti huwa zinatupwa.

Walijua kwenye eneo hilo hawatachukua muda, mizimu itawakimbiza.

Walikubali eneo hilo na kujenga kanisa. Wanakijiji wakawa wanasubiria kwamba watakufa au kukimbia, lakini hilo halikutokea.

Wengi walipoona wamishionari hao hawadhuriki kwa mizimu hiyo, waliwaamini na kujiunga nao. Nwoye pia alijiunga nao na baba yake alipopata taarifa alimwadhibu, Nwoye aliondoka na hakurudi tena.

Alienda kanisani na kueleza kwamba ameamua kujiunga na kanisa moja kwa moja, alipokelewa vizuri na kupelekwa Umuofia ambapo kanisa lilikuwa limeanzisha shule ya kuwafundisha kusoma na kuandika.

Okonkwo alisikitishwa sana kuwa na mtoto wa aina hiyo, anayeiacha miungu ya baba yake na kufuata mungu wa wazungu.

👉18

Kanisa linaendelea kukua na kupata wafuasi. Watu wote waliotengwa kwenye jamii wanapokelewa na kanisa.

Kiongozi wa kanisa aliyewekwa na wamishionari wazungu anawaambia waumini wengine wawakubali watu wote kwa kuwa mbele za mungu watu wote ni sawa.

Mwanzo hakukuwa na mgogoro kati ya kanisa na kijiji, kwa kuwa kanisa lilikuwa kwenye msitu wa mizimu.

Lakini baadaye baadhi ya waumini walianza kuingia kijijini na kubadili baadhi ya mambo.

Mmoja alimuua nyoka anayeheshimika sana na ndiye mungu wa maji. Wazee wanakaa na kuamua wote waliojiunga na kanisa watengwe na kijiji, wasiruhusiwe kutumia kitu chochote cha kijiji.

👉19

Mwaka wa mwisho wa Okonkwo kuwa uhamishoni umefika.

Kwa miaka saba amekuwa kijiji cha Mbanta, amepata mafanikio makubwa, lakini anaamini angekuwa amepiga hatua zaidi iwapo angekuwa kijijini kwake Umuofia.

Anatuma fedha kwa rafiki yake Obierika amjengee nyuma ya kushukia anaporudi.

Anaandaa sherehe kubwa ya kuwaaga watu wa Mbanta na kuwashukuru kwa kumpokea vizuri.

Wazee wanamshukuru pia kwa sherehe kubwa aliyowaandalia, wanamwambia lengo la sherehe siyo kula na kunywa, bali kuja pamoja kama ndugu.

Wanasema wanahofia kizazi cha sasa kimekosa ule ukaribu wa ndugu ndiyo maana wamishionari ni rahisi kuwashawishi na wakabadili imani zao.

👉20

Okonkwo anarudi Umuofia, anakuta mambo mengi mno yamebadilika.

Kanisa limekuwa na wafuasi wengi na mpaka baadhi ya wazee wenye heshima wamejiunga nalo.

Pamoja na kanisa, wazungu pia wameleta serikali, mahakama na gereza.

Wale wanaovunja sheria wanahukumiwa na kisha kufungwa au kunyongwa.

Okonkwo anasikitishwa na jinsi kijiji chake kimeruhusu hayo kutokea.

Anazungumza na rafiki yake Obierika na kumuuliza kwa nini wasifanye kitu kuwaondoa wazungu hao.

Obierika anamjibu tatizo siyo wazungu, bali wanakijiji wenzao ambao wameshatekwa na kuwaamini wazungu hao.

Obierika anamueleza kwamba wazungu hao ni wajanja, walipokuja waliona hawana madhara kwa kuwa ni wachache, ila sasa wana wafuasi wengi kiasi kwamba kuwatoa ni vigumu.

👉21

Mmishionari mkuu Mr. Brown amekuwa akiwasisitiza wafuasi wake kutokudharau mila za wanakijiji.

Amekuwa anajenga mahusiano mazuri na wazee wa kijiji, wakijadiliana kuhusu tofauti ya imani zao.

Kupitia mijadala hiyo, Mr. Brown anajifunza kwamba matumizi ya nguvu hayatamsaidia kupata wafuasi zaidi.

Hivyo anatumia njia nyingine, anajenga shule na hospitali na kuwashawishi watu watumie huduma

hizo.

Mwanzo wazazi hawakutaka kuwapeleka watoto wao kwenye shule hizo, ila aliwashawishi kwamba kama hawatafanya hivyo, watatawaliwa na watu kutoka maeneo mengine.

Shule zilianza kupata wanafunzi wengi na hata hospitali pia, sifa ikisambaa kwamba dawa za mzungu zinafanya kazi haraka.

Mr. Brown aliomba kuonana na Okonkwo lakini akakataa, mtoto wake Nwoye ameenda chuo cha ualimu, lakini Okonkwo hajali chochote kuhusu mtoto huyo, kwani alishamkataa siyo mtoto wake. Tangu Okonkwo amerudi amekuwa na mawazo sana, hii siyo Umuofia aliyoiijua, iliyokuwa inahifiwa kwa ushujaa.

Aliona jamii yake inaanguka na wamishionari wanapata nguvu kubwa, kitu kilichomuumiza sana. Pia alipokuwa anarudi alitegemea kujenga upya jina lake na kupata vyeo vya kijamii vitakavyomfanya ajulikane, lakini mambo hayajawa hivyo. Hakuna anayejali sana kuhusu kurudi kwake, wengi wanafuatilia zaidi mambo ya wamishionari.

👉22

Mr. Brown anapata changamoto ya kiafya na kuondoka Umuofia, anakuja Mr. Smith kuchukua nafasi yake.

Mr. Smith alidharau mbinu alizokuwa anatumia Mr. Brown, aliona ni mbinu za upole ambazo haziwezi kukuza kanisa.

Hivyo yeye alikuja na mbinu za imani kali na kupinga mila zote za asili.

Muumini mmoja anaoenda kwenye mkusanyiko wa mizimu ya kijiji na kuwadharau kwamba hawawezi kufanya chochote.

Wazee wanakasirishwa na mizimu hiyo inaenda kuchoma kanisa moto, huku ikiwambia Mr. Smith kwamba hawatamduru, kwa sababu walimheshimu Mr. Brown.

Ila wanamwambia kama anataka kuendelea kukaa Umuofia basi aache kuingilia mila zao, anaweza kuabudu mungu wake atakavyo, ila asiingilie miungu ya asili yao.

👉23

Siki chache baada ya kanisa kuchomwa, hakimumu anatumia ujumbe wa kukutana na wazee wa Umuofia. Wazee sita wanaenda, Okonkwo akiwa mmoja wao ambaye anawatahadharisha wabebe silaha, mtu mweupe siyo wa kuamini.

Wanafika kwenye mahakama, hakimumu anawaambia amesikia kilichotokea, hivyo amewaita wajiadiliane namna ya kuzuia hilo lisitokee tena.

Mzee mmoja anasimama kuongea, hakimumu anamtaka asubiri ili watu wake waingie na kusikiliza pia.

Wanaingia watu 12 ambao wanakaa pamoja na wazee wale na ghafla wazee wanajikuta wamefungwa pingu.

Hawakujua hata imetokeaje, hakimumu anawaambia wamekuwa wakinyanyasa watu na wamechoma nyumba za watu na kanisa pia. Hata kama mtu amekosea hawapaswi kuchukua sheria mikononi, wanapaswa kwenda kushitaki.

Anawapiga faini ya kulipa fedha ndiyo waachiliwe, la sivyo watanyongwa.

Anawauliza kama wana la kujitetea, wote wanakaa kimya.

Wanawekwa mbaroni kwa siku tatu bila kula wala kunywa, mlinzi anayewalinda anawadhihaki na kuwapiga.

Wanakijiji wanakutana na kuamua kuchanga fedha ili waweze kuwatoa wazee hao kabla hawajaenda kunyongwa.

👉24

Faini inalipwa na wazee sita wanaachiliwa.

Wanarudi kijijini wakiwa kimya na wenye huzuni.

Okonkwo anafika nyumbani kwake, mgongo wake unauma baada ya kuumizwa na kipigo cha mlinzi aliyekuwa anawalinda.

Anaapa kulipa kisasi, hata kama wenzake hawatakubali, yeye lazima aliipe kisasi.

La mgambo linalia, kesho kutakuwa na mkutano wa wanakijiji wote.

Okonkwo anapata matumaini, anaona kuna nafasi ya kuchukua hatua. Anajiambia atawashawishi wazee wengine wakubali kuingia vitani kuwaondoa wamishionari hao.

Siku ya mkutano inafika, wanakijiji wanakusanyika na wazee wanaanza kuongea. Wa kwanza anaongea na kumaliza.

Wapili anaongea kueleza jinsi wamishionari walivyoharibu kila kitu cha Umuofia, anawataka wanakijiji wenzake waungane kupigana vita kuwaondoa wamishionari hao.

Kabla hajamaliza kuongea wanakuja maaskari kutoka kwa hakimumu. Okonkwo anamtambua yule aliyemuumiza, anamuuliza amefuata nini, anajibu hakimumu ameagiza mkutano huo usitishwe mara moja.

Kwa hasira Okonkwo anatoa panga lake na kumkata askari yule, anadondoka chini na kufa.

Wenzake wanne wanaondoka na hapo Okonkwo anajiambia wanakijiji hao hawapo tayari kwa vita, kwani wangukuwa tayari wasingewaacha askari hao wengine waondoke.

Anaondoka kurudi nyumbani kwake.

👉25

Hakimu anaenda na wanajeshi nyumbani kwa Okonkwo, anakuta watu wamekaa kwa huzuni wakiongea.

Anauliza nani kati yenu ni Okonkwo, Obierika anajibu Okonkwo hayuko hapa.

Hakimu anauliza yuko wapi, wanamjibu wanaweza kumpeleka alipo, ila pia wataomba msaada wao.

Wanawapeleka mpaka kwenye mti mkubwa ambapo mwili wa Okonkwo ulikuwa unaning'inia.

Obierika anamwambia hakimumu, huyu alikuwa mmoja wa watu wakuu na mashujaa wa Umuofia, umepelelea mpaka amejinyinga na sasa atazikwa kama mbwa.

Obierika anawaambia kwa tamaduni zao mtu aliyejinyonga huwa haguswi na watu wa kabila lake na hazikwi kwa heshima.

Hivyo wanaomba wawasaidia kushusha mwili huo na kwenda kuuzika na watawalipa.

Hakimu anaeleza mwili ushushwe na kupelekwa mahakamani pamoja na watu wale.

👉SOMO.

Things fall apart ni moja ya riwaya zinazoelezea mapambano yaliyokuwepo wakati wa kuja kwa ukoloni Afrika.

Mgongano wa imani na tamaduni ulivyoleta machafuko na mauaji kwenye maeneo mengi.

Kuna mengi ya kujifunza hata sasa kwenye maisha tunayoishi ili tuweze kuwa na maisha bora.

Baadhi ya yale muhimu tunayoweza kuondoka nayo hapa ni;

1. Umuhimu wa kupambana ili kufanikiwa kwenye maisha. Tumeona jinsi Okonkwo alivyokuwa mpamnaji.

2. Hata kama huna pa kuanzia, ukiwa na juhudi watu watakuamini na kukupa fursa nzuri. Juhudi za Okonkwo zilimfanya aaminike.

3. Watoto hawalingani na wala hawawezi kufanana na wazazi. Tumeona Okonkwo akikazana kumfanya mtoto wake Nwoye awe kama yeye, kitu kinachoshindikana.

4. Baadhi ya imani ni potofu na zinaleta ukandamizaji kwa wengine. Imani nyingi za Umuofia kama kuua mapacha, kutenga walio tofauti hazikuwa na maana.

5. Matumizi ya mabavu siyo mazuri kwenye kuwashawishi watu. Tunaona mmishionari Mr. Brown alitumia njia ya upole na maelewano kuwashawishi watu na ikafanikiwa bila kuleta machafuko. Ila Mr. Smith alitumia mabavu na yakaleta machafuko.

6. Hata kama unapitia magumu kiasi gani, usikate tamaa, jipe muda na fanya kilicho sahihi na utayavuka. Mwanzo wa kuishi uhamishoni Okonkwo alikuwa amekata tamaa, ila baada ya kusemwa na mjomba wake aliamua maisha yaende na akamaliza miaka saba ya adhabu kwa mafanikio makubwa.

7. Kuna mabadiliko yakitokea mambo hayawezi kurudi tena nyuma, unapaswa kukubaliana na mabadiliko hayo. Okonkwo alitamani sana Umuofia ya nyuma irudi, lakini alishachelewa, mambo

yalikuwa yamebadilika sana.

8. Tunahitaji marafiki wa kweli kwenye maisha, walio tayari kutusaidia kwa kila namna. Tumeona jinsi Obierika alivyokuwa msaada mkubwa kwa Okonkwo, tangu adhabu ya kukaa uhamishoni, kurudi kwake na mpaka kifo chake.

9. Kuonesha hisia siyo udhaifu, tumeona jinsi ambavyo Okonkwo alikuwa na hisia za upendo ndani yake, lakini alizificha akiamini kuzionesha ni udhaifu, kitu kilichomtesa binafsi na kujenga mahusiano mabovu na mtoto wake wa kwanza.

10. Siyo lazima uthibitishe kila wakati wewe ni shujaa, ushujaa wako unajulikana kwa matendo na misingi unayoiishi na siyo kujionesha. Okonkwo alitahadharishwa asishiriki kwenye kumtoa kafara Ikemefuna, lakini alitaka kuonekana shujaa na akamuua mwenyewe, kitu ambacho kilimtesa kwa muda mrefu na hata kuharibu mahusiano yake na mtoto wake Nwoye.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,

www.t.me/somavitabutanania